# OFISI YA RAISI
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## KAMATI YA MITIHANI YA SHULE ZASEKONDARI SAME NA MWANGA (SAMWASSES)

## MTIHANI WA KABLA YA MTIHANI WA UTAMIRIFU
### KISWAHILI 02
### MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

1. Mtahiniwa anatakiwa afafanue faida tatu za matambiko na hasara mbili za matambiko katika jamii, kam a ifuatavyo:

<u>FAIDA ZA TAMBIKO</u>

⇒ Tambiko hujenga jamii kama chombo cha kutatulia matatizo katika jamii. Jamii ya asili ilipokabiliwa na matatizo ilifanya tambiko na kusali ili miungu iwasaidie kuondoana na tatizo hilo.

⇒ Tambiko husaidia kuendeleza mila na desturi za jamii.

⇒ Tambiko hujenga na kuimarisha mahusiano miongoni mwa jamii.

⇒ Matambiko huiongoza jamii katika mapambano dhidi ya matatizo mbalimbali yanayowakabili.

<u>HASARA ZA TAMBIKO</u>

⇒ Hujenga dhana potofu katika jamii. Tambiko hufanya watu kuamini nguvu Fulani bila kuwa na uhakika au uthibitisho wa kisayansi.

⇒ Huleta hasara kubwa za kiuchumi ka jamii. Kafara ya tambiko inahitaji mnyama au chakula, ambapo watu hutumia pesa nyingi kuvipata vitu hivyo.

$utanguliz\ alama\ 01\ Kiin\ \ 4\ @\ 2\ =\ alama\ 08\ Hitimishoalama\ 01\ \}JUMLA\ =\ alama\ 10$

2. Mtahiniwa afafanue mihula mine ya maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa mujibu wa wataalamu kama ifuatavyo:-

i) Mhula wa urasimu
Ni kipindi maalumu ambacho ndo msingi wa kuwekwa kwa sheria au kanuni za jambo Fulani. Urasimi wa ushairi wa Kiswahili ulipata mashiko mnamo karne ya 18 (1700-1800) katika kipindi hicho kulikuwa na tungo kama utenzi wa Tambuko.

ii) Muhula wa utasa.
Kipindi hiki kiliitwa utasa kwa sababu kulikuwa bna ukame wa tungo kwa takriban miongo mitatu (1885-1945) Tungo zilikuwa chache kwa sababu ya matukio ya vita.

iii) Muhula wa urasimi mpya.
Ulishuhudia kuimarishwa kwa kanuni za utungaji wa ushairi wa Kiswahili, mf. Sheria ya kanuni ya utunzi wa diwani ya shabani Robert.

iv) Muhula wa usasa
Ulianza baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kupata uhuru katika kipindi hiki kulikuwa na wasomaji wengi ngazi ya chuo kikuu.

$alama\ 4\ @\ 02\frac{1}{2} = alama\ 10$

3. Mtahinia anatakia afafanue mambo yaliyosababisha ushairi kukua na kuenea kabla na baada ya uhuru baadhi ya mambo hayo ni kama vile:

i) Dini ya kiislamu na kikristo

ii) Hati za kiarabu na kirumi

iii) harakati za kisiasa

iv) Suala la elimu

v) Vyombo vya habari, mf. Magazeti

vi) Tafiti mbalimbali kuhusu utanzu wa ushairi.

$alama\ 5\ @\ 02 = alama\ 10$

4. Mtahiniwa asome habari aliyopewa kasha ajadili mbinu za kifani zilizotumika kama ifuatavyo:

a) Muundo
Mwandishi ametumia muundo wa msago (yaani moja kwa moja ameanza na Eva tangu mwanzo anapoamka hadi kuhudhuria mkutano).

b) Mtindo – masimulizi

c) Mandhari
Mandhari ya kijijini lakini pia zinataja sehemu zingine mf. Sehemu ya mkutano.

d) Wahusika:
Eva, Jero, mzee mpuo, mzee kolwa na mzee Kenge.

e) Matumii ya Lugha.
   - Tamathali za semi
   - Tashibiha – walikaa kimya kama wamepigwa
     - Aliingiwa na woga kama wasasi
   - Takriri – kinyumenyume
   - Misemo na Nahau - Kumkodolea macho
     - Kuchapua mwendo.

$alama\ 5\ @\ 02\ =\ alama\ 10$

5. Mtahiniwa aoneshe namna matumizi ya mitindo yanayoonesha umahiri wa waandishi.Baadhi ya mitindo hiyo ni ;

- Chungu Tamu
  i) Mtindo wa masimulizi umetumika Mfano ‘’Chatu na Kuku ‘Daktari Askari’ Thomas na Dotto’Manzese mpaka Ostabei’’

  ii) Mtindo wa amri .Kuamrisha juu jambo lolote lenye manufaa katika jamii.Katika shairi la ‘’Usiwe Mwonja Asali’’

  iii) Mtindo wa ulinganifu wa vina na mizani;diwani hii ina ulinganifu huu,kwa kawaida mashairi hayo yana mizani kumi na sita .Mfano ‘Chini ya mti Mkavu ‘

  iv) Mtindo wa kidatu; katika mtindo huu baadhi ya mistari hufupisha maneno au silabi tofauti na mstari mwingine ambayo huwa na silabi au maneno mengi Mfano .’chatu na kuku;

  v) Mtindo wa nafsi ; huu ni mtindo ambao mwandishi anaweza kutumia nafsi umoja na nafsi wingi au kikundi .kwa mafano ‘;wanajua kuvumila ;

- Fungate ya Uhuru
  i) Mtindo wa mizani na vina ;Baadhi ya mashairi ya diwani hii yana ulinganifu wa vina na mizani. Kwa mfano ,;Kunta sauti ya Kiza ;(uk.33)

  ii) Mtindo wa kiitikio /kibwangizo (kituo) ;huu ni mtindo ambao mstari wa mwisho hujirudia rudia kwa kila ubeti wa shairi zima .Kwa mfano ,;Dfina ‘( uk.8-10)

  iii) Mtindo wa kuhoji ; ni mtindo unaotumiwa na mwandishi kuuliza maswali ambayo aidha majibu yake yako wazi au hayako wazi .Mara nyingi mtindo huu hutumika kama kejeli au dhihaka .’Tumesalitwa’’(uk.5)’’Si wewe ‘’(uk.38)

  iv) Mtindo wa kidatu ; katika mtindo huu wa kidatu ,baadhi ya mistari au mstari hufupisha maneno mengi .Kwa mafano ,; Nahodha Mtwesi ;(uk.6)Mjamzito (uk7-8)

  v) Mtindo wa nafsi ; ni mtindo ambao mwandishi anaweza kutumia nafsi moja au wingi au kikundi . Kila nafsi ina maana yake kimaudhui.’’Nikizipata Bunduki’’(uk.11-12).’’Gorila’’(14-15)

  $utangul\quad alama\ 02\ Kiin\ \ hoja\ 8\ @\ 2\ =\ alama\ 16\ Hitimisho\quad alama\ 02\ \}JUMLA\ =\ alama$

6. Mtahiniwa aeleze maana ya shairi guni.
   - Ni mashairi yanayofuata kanuni ya urari wa viria na miani, mashairi hayo pia yanaitwa mapingiti.
   - Mashairi ghani si kuburudisha tu bali yanatia mafunzo na ujumbe.

   CHUNGU TAMU
   - Matabaka ni kikwazo cha maendeleo ya jamii
   - Uongozi mbaya ni kikwazo cha ujenzi wa jamii
   - Demokrasia ya kweli ndio inayotakiwa.
   - Mapenzi yaachiwe wanaopendana

   FUNGATE YA UHURU
   - Uongozi ni kikwazo cha maendeleo ya jamii.
   - Umoja na mshikamano ni njia ya ujenzi wa jamii mpya
   - Ukoloni mamboleo ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya
   - Ufasiri ni kujitoa muhanga lni njia ya kufanya mapinduzi.
   - Mapenzi ya kweli ndio yanayotakiwa katika jamii.

$$utangul \quad alama\ 02\ Kiin \ \ alama\ 8\ @\ 2\ =\ alama\ 16\ Hitimisho \quad alama\ 02\ \}JUMLA\ =\ alama\ 20$$

7. Mandhari ni mahali au sehemu kazi ya fasihi inapotendeka.
   - Mtahiniwa aeleze ni kwa namna gani mandhari yalivyoweza kufikisha ujumbe kwa jamii.

   VUTA N’KUVUTE
   i) Mandhari ya chumba cha Denge: kilikuwa kimetapakaa makaratasi mbalimbali ambayo ni kokezo kuwa harakati za ukombozi halikuwa jambo jepesi.

   ii) Mandhari ya gerezani: inabeba kuwa uvumilivu na lujasiri ni mbinu muhimu za kujikomboa

   iii) Mandhari ya nyumbani kwa shihabu: inabeba ujumbe kuwa utawa ni kikwazo cha maendeleo ya mwanamke.

   iv) Mandhari ya karemjee club: inawakilisha matabaka ambapo huko ndiko wakoloni walipokuwa wakijiburudisha.

   MFADHILI
   i) Mandari y ofisini: hapa tunaona ofisini kwa Gadi Bulla Arusha ambapo tunapata ujumbe wa uzembe kazini pale aliposaini hundi ya malipo hewa.

   ii) Mandhari ya nyumbani: kuna ujumbe wa mapenzi ya dhati kati ya bi Hununa na mdogo wake, manzi ya ulaghai kati ya Nyambuja na Gadi Bullah.

   iii) Mandhari ya barabarani; inatupa ujumbe wa ujasiri aliokuwa nao Nunu, pindi walipozuiwa na askari w barabarani alionesha ujasiri wa hali ya juu sana katika kujibizana na yule askari.

   iv) Mandhari ya hospitalini; hapa tunapata ujumbe wa ujasiri na huruma alivyovionyesha Gadi Bullah wa kujitolea figo yake kwaajili ya Dania.

$utangul \quad alama\ 02\ Kiin\ \ 8\ @\ 2\ =\ alama\ 16\ Hitimisho \quad alama\ 02\ \}JUMLA\ =\ alama\ 20$

8. Mtahiniwa aonyeshe jinsi kipengele cha semi kinavyotumika katika tamthiliya mbili ambapo anapaswa kufafanua vipera vitatu kwa kila kitabu.

MORANI

⇒ Methali
- penye nia pana njia
- subira yavuta heri
- Siri ya kaburi anajua maiti

⇒ Nahaha
- anatuchoma utambi
- ndumila kuwili

⇒ Misemo
- paka shule
- ameota meno jana.

NGUZO MAMA

⇒ Methali
- La mgambo likilia kuna jambo
- Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
- Asiye na mwana aeleke jiwe.

⇒ Nahau
- Utakuja kibwelu
- Akachanganya ulimi.

⇒ Misemo
- Watoto taifa la kesho
- utakiona cha mtema kuni

$utangul \quad alama\ 02\ Kiin\ \ 8\ @\ 2\ =\ alama\ 16\ Hitimisho \quad alama\ 02\ \}JUMLA\ =\ alama\ 20$